



JARIDA LA WIKI NOVEMBA 1 HADI NOVEMBA 7,2021

SERIKALI YATOA MIL.250 ZA UPANUZI WA ZAHANATI YA UFUKONI KUWA KITUO CHA AFYA



**MILIONI 250 ZA TOZO YA MIAMALA
YA SIMU ZATOLEWA KWA AJILI YA
UPANUZI WA ZAHANATI YA UFUKONI
KUWA KITUO CHA AFYA.**



 Mtwara-Mikindani Mc
 Mtwara Mikindani Manispaa
 mtwaramikindanime
WWW.mtwaramikindanime.go.tz

Kutokana na Zahanati ya Ufukoni kuhudumia idadi kubwa ya watu kuliko zahanati nyingine zilizopo Manispaa ya Mtwara-Mikindani , Serikali kupitia tozo za miamala ya simu iliyoanza Julai mwaka huu imetuletea shilingi 250,000,000 kwa ajili ya upanuzi wa Zahanati ya Ufukoni ili kuwa Kituo cha afya.

Mkuu wa Shule apongezwa Kushirikisha Wanafunzi Kwenye Ujenzi.



Mkuu Wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Dunstan Kyobya amempongeza Mkuu wa Shule ya Sekondari ya

Ufundi Mtwara kwa kutumia ubunifu wa kuwashirikisha wanafunzi wa shule hiyo katika ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili vinavyojengwa shuleni hapo kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

“Nikupongeze huu ni ubunifu mkubwa umeonesha, hawajifunzi tu kwa vitendo lakini wamepata somo la kuwa wazalendo” Amesema Kyobya

Mhe . Kyobya ametoa pongezi hizo Novemba 4,2021 katika Ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Mtwara ilipotembelea kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa madarasa yanaoyojengwa kupitia Mpango wa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Amesema kuwa ubunifu huo ni funzo kubwa la ushirikishwaji wa wananchi na kusisitiza kuwa ushirikishwaji wa wanafunzi hao hautaathiri ubora wa

madarasa hayo kwa kuwa kuna wataalam wanaosimamia ujenzi huo.

Ili kukamilisha madarasa hayo kwa wakati na kwa ubora unaohitajika Mhe. Kyobya amemtaka Diwani wa Kata ya Shangani Mhe. Abuu Mohamedi kuendelea kutoa hamasa kwa wananchi wa Kata hiyo ili kushiriki katika ujenzi huo.

Kwa Upande wake Diwani wa Kata ya Shangani Mhe. Abuu Mohamed amemhakikishia Mhe. Kyobya kumaliza ujenzi wa madarasa hayo ndani ya Muda uliopangwa na katika ubora zaidi.

Naye Asha Jumanne Mwanafunzi wa Kidato cha Pili katika Shule ya Ufundi Mtwara amemshukuru Rais Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassani kwa kupunguza changamoto ya madarasa katika Shule yao.

Kamati hiyo imetembelea Ujenzi wa vyumba vya madarasa Sekondari ya Sabasaba, Bandari, Shangani, Chuno, Magomeni, Mitengo, Mangamba na Naliendele .

Kamati Za Ujenzi Za Shule Zashauriwa Kununua Vifaa Viwandani

Ikiwa zimepita siku 25 tangu Uzinduzi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 uzinduliwe jijini Dodoma na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan, na Manispaa ya Mtwara-Mikindani kupokea kiasi cha 440,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba ishirini na mbili vya madarasa kwa shule za Sekondari, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Dunstan Kyobya amewataka wajumbe wa Kamati za manunuzi katika ujenzi huo kuhakikisha wananunua vifaa vya ujenzi kutoka viwandani ili kupunguza gharama za ujenzi.

“Ukinunua bidhaa toka viwandani inapunguza gharama na pia unaweza kusevu hela ambayo unaweza kuitumia katika miradi mingine mfano hata ujenzi wa ofisi za wali-mu” Amesema Kyobya

Mhe. Kyobya ametoa rai hiyo Novemba 4, 2021 katika Ziara ya Kamati Kuu ya Mkoa wa Mtwara ilipotembelea kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa vyumba vya madarasa vinavyojengwa kupitia

fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 katika Manispaa Aidha amewataka wajumbe hao kuzingatia ubora katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi lakini pia ku-shirikiana katika utendaji wao ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao katika ujenzi huo.

Kwa Upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani Bi. Tamko Ally amesema kuwa tayari ofisi yake imeshaanza utekelezaji wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi toka viwandani ambapo saruji inayotumika katika ujenzi huo imeagizwa kutoka katika kiwanda cha saruji Dangote.

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na amemhakikishia kuwa madarasa hayo yatakamilika ndani ya muda uliopangwa.





Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Dunstan Kyobya (aliyevaa kofia) akizungumza na wananchi wa Kata ya Ufukoni alipotembelea Zahanati ya Ufukoni Novemba 4,2021.

Baada ya Zahanati ya Ufukoni kupokea fedha kutoka Serikali kuu kiasi cha Tsh. **250,000,000** kwa ajili ya Upanuzi wa Zahanati hiyo kuwa Kituo cha Afya, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Dunstan Kyobya amemuagiza Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani Bi. Tamko Ally kuharakisha mchakato wa ununuzi wa vifaa kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya Zahanati hiyo ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

Amesema kuwa uchelewaji wa ununuzi wa vifaa utapelekea ujenzi huo kutokamilika kwa wakati na kusababisha adha kwa wananchi kuendelea kufuata huduma katika maeneo mengine.

Mhe. Kyobya ametoa agizo Novemba 4,2021 katika Ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ilipotembelea kukagua Utekelezaji wa Ujenzi wa Madarasa katika Manispaa yetu.

Aidha amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika ujenzi huo ili kuiongezea nguvu Serikali.

“Kama tulivyoshirikiana katika miradi mingine nawaomba tujitokeze kushiriki kimamilifu maana hiki Kituo cha Afya ni cha sisi wananchi”Amesema Kyobya

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani Bi. Tamko Ally amemhakikishia Mhe. Kyobya kuwa mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi utaharakishwa kama alivyoagiza.

Bi. Salima Namenya Mkazi wa Kata ya Ufukoni amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Mhungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha za upanuzi wa Zahanati ya Ufukoni kuwa Kituo cha Afya kwani Kituo hicho kitapanua wigo katika utoaji wa huduma za Afya.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



TAARIFA KWA UMMA.

**MAPOKEZI YA FEDHA MIL. 250 ZA UPANUZI WA ZAHANATI YA UFUKONI KUWA KIT-
UO CHA AFYA.**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani Col. Emanuel Mwaigobeko anapenda kuutaarifu umma kuwa Ofisi yake imepokea fedha Tsh. 250,000,000 (**Shilingi milioni mia mbili hamsini**) kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya upanuzi wa Zahanati ya Ufukoni kuwa Kituo cha afya.

Fedha za upanuzi wa Zahanati ya Ufukoni zimetokana na tozo za miamala ya simu iliyoanza Julai mwaka huu na tayari zimeshaingizwa kwenye akaunti ya Manispaa kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya afya ikiwemo:-

- i. Jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje (OPD)
- ii. Jengo la Maabara (Laboratory)
- iii. Kichomea taka (Incinerator).

Zahanati ya Ufukoni inapanuliwa kuwa Kituo cha afya kwa kuwa zahanati hii kwa sasa inahudumia idadi kubwa ya watu ukilinganisha na zahanati zingine zilizopo Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Jamadi A. Omari

Afisa Habari

Manispaa ya Mtwara-Mikindani

2/11/2021.

MATUKIO KATIKA PICHA



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani akishiriki Bi. Shadida Ndiile akishiriki Kuchanganya zege la ujenzi wa Msingi wa madarasa mawili ya Sekondari ya Mtwara-Ufundi



Kamanda wa Polisi Wilaya ya Mtwara SSP Obbaso Nguvila kishiriki kuchimba Msingi wa madarasa mawili Sekondari ya Shangani



Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Dunstan akisalimiana na Mkuu ya Shule ya Sekondari ya Mtwara-Ufundi Riyadh Kadhi ali-potembelea shuleni hapo Novemba 4,2021

